Students Name: ……………………………………………………………………………

School Name………………………………………… Index Number ……………

**336/1**
KISWAHILI
PAPER 1
JULY/AUGUST 2025
2 HOURS

# HES MOCK EXAMINATIONS 2025

## UGANDA CERTIFICATE OF EDUCATION

## KISWAHILI

## KARATASI YA KWANZA

## 2 HOURS

**MAAGIZO**

- Jibu maswali mawili kwa jumla
- Sehemu A katika sehemu hii kuna maswali mawili chagua swali moja
- Sehemu B ni ya lazima kwa watahiniwa wote.

## SEHEMU A (INSHA)

## AMA

1. a) Majanga ni maafa yanayojitokeza kidharura kuharibu mazingira. Kuna sehemu nyingi chini Uganda ambazo zimekumbwa na Majanga tofauti. Pia, Majanga haya yana vyanzo vingi nchini Uganda. Binadamu anaweza kuweka njia tofauti za kuzuia/kusuluhisha Majanga. Andika insha Ukieleza njia Kadhaa za kutatua tatizo hili nchini Uganda.

**AU**

2. b) Hali na vitendo vya kizalendo havifai kudhihirika kwa viongozi tu ila ni wajibu wa kila mtu kuwa mzalendo katika nchi yake. Umechanguliwa na mwalimu mkuu wa shule yako kuwahamasisha wanafunzi wenzako kuhusu jinsi ya kuishi kama wazalendo katika jamii zenu Katika nchi yenu.
   Andika hotuba ambayo utawasilisha kwenye mkusanyiko wa wanafunzi wote katika shule yako ukiwahimiza kuwa wazalendo na pia kuwa elezea umuhimu wa uzalendo.

## SEHEMU YA B

## UFUPISHO

3. Kwa kutumia maneno themanini (80) eleza umuhimu wa mwalimu katika maisha ya kila mwanafunzi maishani.

Bila shaka umewahi kusikia neno, mwalimu likitajwa. Je neno hili linapotajwa ni wazo gani hukuja akilini? Yamkini huenda ukaniambia kwamba mwalimu ni yule ambaye anakufundisha masomo mbalimbali darasani. Wengine huenda anawaridhisha wengine maarifa, yawe ya darasani au nje ya darasa. Alimradi kila binadamu anaweza kutoa maana anuwai za neno hili kulingana na namna ambavyo aliathiriwa na mwalimu.

Mwalimu ni mtu yeyote mwenye ujuzi, ambaye anaupitisha ujuzi huo kwa mtu mwingine mwenye kiwango cha chini cha ujuzi. Hakika hata wewe mwanafunzi umewahi kuwa mwalimu kwa mwanafunzi mwenzako au hata mwalimu wako! Fikiria mkiwa kwa darasa la kwanza au la pili namna ulivyomfundisha mwanafunzi mwenzako namna ya kuchora

maumbo mbalimbali, kuruka kamba, na hata kufunga tai. Huenda ukadhani kwamba hujawahi kumfundisha mwalimu wako lolote. Hatahivyo, kumbuka kwamba wakati unapochangia somo lolote darasani huwa unawafunza wengine, akiwemo mwalimu kuhusu namna ya kueleza mambo tofauti. Pia unaweza hata kumfuza mwalimu wako maarifa mapya. Mathalani unapopewa fursa ya kuwasimulia wenzako hadithi kutoka jamii yako unapata fursa ya kumfunza mwalimu na mwanafunzi wenzako kuhusu utamaduni wa jamii yako. Kupitia hadithi fursa ya kumfunza mwalimu na mwanafunzi wenzako kuhusu utamaduni wa jamii yako. Kupitia hadithi hizi unaweza pia kufunza namna ya utambaji.

Umuhimu wa mwalimu yeyote yule hauwezi kupuuzwa. Mwalimu humwondolea mtu ujinga kwa kumfunza maarifa mbalimbali. Wewe fikiria ulipongia katika shule ya chekechea. Ulikuwa mgeni kabisa katika mazingira ya shule. Ulikuwa hujazoea kuishi na watu ambao si familia yako. Jambo la kwanza ya kuishi na wengine, alikufunza pia namna ya na kushirikiana nao katika michezo mbalimbali bila kuumizana. Juu ya hayo, mwalimu alikufunza namna ya kutamka sauti na maneno mbalimbali. Baadaye alikufunza pia kuandika na kuwasiliana kwa mtindo anuwai.

Licha ya kusoma masomo mbalimbali mwalimu huelekeza kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri masomo ya mwanafunzi. Hushauri namna ya kutafuta haki na kusuluhisha migogoro kwa Amani. Mwalimu hukushauri kwamba hata mwenzako anapokukosea haufai kumtusi au kumwendea mwalimu kumshataki. Njia bora ni kumwambia kwa utulivu kuwa amekosea na kumsamehe iwapo atakuomba mshaha. Ikiwa mwenzako atashindwa kuona kosa alilokutenda basi unaweza kumwambia mwalimu ili walekeze Zaidi na kuwasaidia kusuluhisha tatizo lenu.

Mwalimu pia hukusudia kutambua na kukuza vipawa vyako, vilevile hukuelekeza kutambua udhaifu wako katika masomo na hali tofautitofauti na kuhimiza kutafuta mikakati ya kujimarisha. Mathalani, ikiwa una kipawa cha ushari mwalimu anaweza kukusaidia kukiimarisha. Hakika wapo washairi stadi ambao walisadiwa kufikia kiwango hiki na mwalimu wao. Vilevile kuna wasusi ambao wameibuka kuwa hodari kwa kusaidiwa na mwalimu wao wa awali katika taaluma ya ususi.

Ni dhahiri kwamba binadamu hukumbana na walimu wengi maishani. Hatahivyo ni muhimu kukumbuka kwamba japo walimu wa kawaida huwa na nia nzuri, wakakufunza ya kukufaa kuna wengine ambao wanaweza kukufunza ya kukushairi. Hawa hawakufunzi kwa maneno tu bali pia kwa vitendo. Walimu wa aina hii hukuvutia kwenye matendo ya kuvitumia vishawishi vingi. Polepole unajikuta umenaswa kabisa ukawa mtumwa wao. Si ajabu kupata kwamba ukiandamana na marafaki ambao wameingilia matumizi mabaya ya madawa ya kulevyo utaishia kuwa mraibu sugu wa madawa hayo, hili hutokea pale ambayo kwa kutaka kujitambulisha na marafiki wako unawafuata namna bendea ifuatavyo upepo. Hivyo basi ni muhimu kuwa na msimamo thabiti hata tunapoingiliana na walimu wa aina mbali mbali tuchuje yanayofaa kujifunza. Yale yasiyofaa tuyaambae kama ukoma.

**MWISHO**